

MAZUNGUMZO

BAINA YA LUQMAN NA OMAR KUHUSU KUSHEREKEA UZAO WA MTUME SALA NA AMANI ZIMFIKIE

MTUNZI

ALFUQAYYIR
ABUU HUDHAYFAT BN ASHURAA



DESIGNER AND PRINTER
ABUU MANSOUR ISSA BNU ISSA

بسم الله الرحمن الرحيم

Shukrani Zote Zinamstaki Allah Subhanahu Wataala , Pia Sala Na Amani Zimfikie Mtume Na Alize Na Masahabaze Na Watakao Fwata Mwenendo Wake Hadi Siku Ya Mwisho , Ama Baada Ya Hayo :

Haya Ni Mazungumzo Ya Kielimu Ya Waislamu Wa Wili , Nimeiita “ Mazungumzo Baina Ya Luqman Na Omar Kuhusu Kusherehekea Uzao Wa Mtume Sala Na Amani Zimfikie “ Ni Risala Ambayo Ni Mwanga Kwa Anaetaka Kujua Haqi , Na Muomba Allah Atuthibitishe Katika Haqi Na Atuongoze Katika Njia İliyo Nyoka .

Mtunzi

Alfuqayyir Abu Hudhayfat Bn Ashuraa

بسم الله الرحمن الرحيم

Tambua Allah Akuhifadhi , Mazungumzo Haya Yatakuwa Ya Kielimu Na Ni Njia Ya Kubainisha Haqi Kwa Aliekuwa Na Shubha Moyoni Mwake , Na Maongezi Haya Mmoja Tutamuita Luqman Ungine Tutamuita Omar .

JE KUSHEREHEKEA UZAO WA MTUME SALA NA AMANİ ZİMFİKİE IMEANZİSHWA NA NANİ ??

-**Anasema Omar:** Assalamun Alaykum Warahmatullahi Wabarakatuh .

-**Anajibu Luqman :** Waalaykumussalam Warahmatullah Wabarakatuh .

-**Anauliza Omar:** Ipi Hukmu Ya Maulidi ?

-**Anajibu Luqman :** Kabla Sijakujibu Kuna Mambo İnabidi Tukubaliyane Nayo kisha Ndipo Tuzungumze Huku Ya Maulidi .

_ Wanawaelimu Wanasema “ Nukta Tutakayo Wafiqiyana Kwayo Ndiyo Tutakayo Anza Kutokea “ , Anasema Abu Zura’ Al Iraqiy Allah Amrehemu : “ Na Wala Hatujui Hilo – Kufanya Maulidi - Hata Kwakulishiza Chakula Kutoka Kwa Wajawema Walio Tangulia “ Tazama Alqaul Alfaswl Fi Hukmi Al ihtifal Bimaulid Khayri Rrusul Karatasi ya 58 .

_ Pia Anasema Assakhawiy Allah Amrehemu : “ Haikunukuliwa Kutoka Kwa yoyote Katika wajawema Waliotangulia Ndani Ya Qarne Tatu Bora …..” Tazama Al Ajwibatul Mardhiyah Fi Sual (Assakhawiy) Anhu Minal Ahadith Annabawiy 1/1116 Namba 316 .

Hapa Tunafaidika Kua Masahaba Na Matabii Na Matabi Tabiina Zama Zao Hapakua Kitu Kinaitwa “ Maulid “ Na Imani Ni Hivo ??

-**Anajibu Omar:** Ndio , Ni Hivo .

-**Anauliza Omar:** Nani Alie Anzisha Maulidi , Na Ni Nani Alie Anza Kusherehekea Maulidi ??

-Anajibu Luqman: Alie Anzisha Maulidi Wanawaelimu Wameikhtilafiyana , Wamoja Wakasema Ni “ Daula Ya Ubaydiyah Alfatwimat “ , Wengine Wakasema Ni “ Abu Said Kuukuburiy – Almalikil Mudhwafar – “ , Wengine Wakasema Ni “ Ashaykhu Omar Bn Muhammad “ , Ama Qauli Sahihi Ni { Daula Ya Ubaydillah Alfatwimat } Ndio Walioweka Na Kulazimisha Watu Kusherehekea Maulidi Ya Mtume Sala Na Amani Zimfikie Kama Alivyo Ashiria “ Almaqriziy Na Qalaqshadiy “ .

_ Ama Alie Anzisha Kusherehekea Maulidi Katika Wa Falme Ni : “ Almuiz Lidini llah Al Fawtimiy “ Tazama Ahsanul Kalam Fima Yataalaq Bissunat Wal Bida’t Minal Ahkam Karatasi Ya 53 .

-Anasema Omar: *Nimefaidika Kuwa Kusherehekea Uzao Wa Mtume Sala Na Amani Zimfikie Halikuwepo Zama Za Mtume Sala Na Amani Zimfikie , Wala Zama Za Masahaba Allah Awaridhie , Wala Zama Za Wanafunzi Wa Masahaba Allah Awaridhie , Wala Zama Za Wanafunzi Wa Wanafunzi Wa Masahaba Allah Awaridhie , Wala İmam Albukhari Na Abu Daud Na Tirmiziy Allah Awaridhie Jambo Hilo Halikuwepo .*

Pia Ni Jambo Ambalo Limezushwa Na Daula Ya Ubaydillah Al Fatwimat Al Batwinat .

-Anasema Omar: Allah Akubarikini , Ni Jibu Hukmu Ya Maulidi Sasa .

Hukmu Ya Kusherehekea Uzao Wa Mtume Sala Na Amani Zimfikie

-Anasema Luqman : Kabla Hujajibiwa Swali Hilo , Je Ni Kila Kitu Alichokiacha Mtume Sala Na Amani Zimfikie Na Masahabaze Kukifanya Kinaleta Maana Ya Katazo – Haijuzu Kukifanya -??

-Anajibu Omar: Si Kila Kitu Alichokiacha Mtume Sala Na Amani Zimfikie Na Masahabaze Kukifanya Kitaleta Maana Ya Katazo Kukifanya .

-Anasema Luqman : Allah Akuwafiqishe Katika Haqi , Umepatia , Sababu Si Kila Alichokiacha Mtume Sala Na Amani Zimfikie Kukifanya İnajuzu Kukifanya Ao Haijuzu Kukifanya Mpaka Tujuwe Ni Jambo Lipi Ameliacha .

_ tambua Allah Akuhifadhi , Mwanaadamu Anamilango Mi Wili , Nayo Ni : “ Mlango Wa Ada “ Na “ Mlango Wa Ibada “ , Kumbe Pindi Tunapoona Mtume Sala Na Amani Zimfikie Ameacha Kufanya Jambo inabidi Tutazame Kaacha Mlango Gani , Je Ni Wa “ Ibada “ Ao “ Ada “ .

Sote Twatambua Kua : Asili Katika Ada Ni Halali Na Ni Mubaha Mpaka Dini Ikukataze , Mfano : Simu , Feni , Gari , Vipaza Sauti Ni Halali Kuvitumia Sababu Sio Ibada . Na Asili Katika Ibada Ni Katazo Kuifanya Ibada Hiyo Mpaka Dini Ikuruhusu .

Je Ewe Omar , Kusherehekea Uzao Wa Mtume Ni Ada Ao Ni Ibada ?? Sababu Hua Wanasema Mwenye Hakwenda Kwenye Uzao Wa Mtume Hampendi Mtume Sala Na Amani Zimfikie , Bali Wanaitikadi Kua Kusherehekea Uzao Wa Mtume Sala Na Amani Zimfikie Anapata Thawabu , Na Wanasema Kua Mwenye Kukataza Kusherehekea Uzao Wa Mtume Sala Na Amani Zimfikie Hamtukuzi Mtume Na Wala Hanusuru Dini .

-Anajibu Omar: Kusherehekea Uzao Wa Mtume Sala Na Amani Zimfikie Ni Ibada .

-Anasema Luqman : Je Mpaka Hapa Bado Hujapata Jibu Kua Kusherehekea Uzao Mtume Sala Na Amani Zimfikie Ni Uzushi ??

-Anasema Omar: Bado Sijakenaika , Naomba Unipe Mwanga Ili Nielewe Zaidi .

-Anasema Luqman : Tambua Allah Akurehemu , Kila Kitendo Ambacho Kilikuwa Na Sababu Katika Zama Za Mtume Sala Na Amani Zimfikie Kisha Mtume Hakukifanya , Je Sunnah Ni Wewe Kukifanya Ao Kukiacha ??

-Anasema Omar: Kukiacha Ndio Sunnah .

-Anasema Luqman : Vile Vile , Kila Ibada Ambayo Masahaba Hawakuijua Hiyo Sio Ibada , Na Kila Uzushi Ni Upotofu , Allah Anasema “ Au hao wana Miungu ya kishirikina walio watungia dini asiyo itolea idhini Allah…… “ Surat Shuura Aya Ya 21 , Law Kama Kusherehekea Uzao Wa Mtume Sala Na Amani Zimfikie İngelikua Ni Kheri Mtume Sala Na Amani Zimfikie Angetuonesha Kua Jambo Hilo İnajuzu , Na Law Kama İngelikua Kusherehekea Uzao Wa Mtume Sala Na Amani Zimfikie Ni Kheri Tungetanguliwa Na Masahaba Kufanya Jambo Hilo .

-Anasema Omar: Ila Nina Dalili Za Kuonesha Kua Kusherehekea Uzao Wa Mtume Sala Na Amani Zimfikie İnajuzu .

-Anasema Luqman : Naam , Nitafurahi Tukatembea Kielimu Ili Upambanukiwe Uhakika Wa Dalili Hizo .

Je Katika Dini Kuna Uzushi Mzuri ??

-Anasema Omar: Je Hujapekuwa Dalili Zinazo Ashiria Kua Katika Dini Kuna Uzushi Mzuri ?

-Anajibu Luqman : Mtume Sala Na Amani Zimfikie Anasema : “ Kila Uzushi Ni Upotofu ..” Imepokewa Na Tirmiziy , Na Anasema

Ibn Omar Allah Awaridhie : “ Kila Uzushi Ni Upotofu , Hata Kama Watu Watauwona Uzushi Huyo Kua Mzuri “ Tazama Al Ibanat Cha Ibn Batwat 1/339 .

_ Anasema Imam Abu Hanifat Allah Amrehemu : “ Ni Juu Yako Kushikamana Na Athar Na Njia Ya Wajawema Waliotangulia , Na Olewako Na Kila Chenye kuzuka , Na kila Chenye Kuzuka Ni Uzushi “ Tazama Dhammul Kalam Wa Ahlihi 1006 .

_ Anasema İman Malik Allah Amrehemu : “ Atakae Zuwa Ndani Ya Uwiislam Uzushi , Akaona Kuwa Uzushi Huyo Ni Mzuri , Atakua Kasema Hakika Muhammad Amefanya Khiyana Katika Ujumbe , Sababu Allah Anasema : “ Leo Nimekukamilishieni Dini Yenu Na Nikatimiza Neema Zangu Na Nika Kururidhieni Uwiislam Kuwa Dini “ . Kile Ambacho Kakikuwa Dini Siku Hiyo , Leo Hakiwezi Kikawa Ni Dini “ Tazama Al Itiswam cha Shatwibiy 1/64 .

-Anasema Omar: Anasema Mtume Sala Na Amani Zimfikie : “ Atakae - سن –Anzisha Katika Uwiislam - سن –Uzushi Mzuri…..” , Hapa Hiyi Hadith Inaashiria Kua Ndani Ya Uwiislam Kuna Uzushi Mzuri .

-Anajibu Luqman : Tambua Allah Akuhifadhi Hiyo Hadith Namna Ulivyo Ifasiri Umekosea , Sababu :

Mtume Sala Na Amani Zimfikie Anasema : “ Atakae Sunnah Miongoni Mwa Sunna Zangu kisha Watu Wa Kaifanyiya Kazi Sunnah hiyo …….” Imepokewa Na Ibn Madjah . Hiyi Ndio Tafsiri Ya Hadith Hiyo .

Pia Hakuna Sahaba Wala Wanafunzi Wa Masahaba Wala Wanafunzi Wa Wanafunzi Wa Masahaba Alitafsiri Kama Ulivyotafsiri , Na Wenyewe Ndio Waliokuwa Wajuzi Wakiarabu Zaidi Yangu Mimi Na Wewe .

Vile Vile Alisema من سن Na Hakusema من ابتدع Atakae Zuwa , Na Akasema في الإسلام Na Uzushi Hauna Nafasi Katika Uwiislam .

-Anasema Omar: Ahsante , Vipi Kuhusu Qauli Ya Omar Bn Khatwab Allah Amridhie : “ Neema Ya Uzushi Ni Huyu “ , Pamoja Na Qauli Ya İmam Shafi’ Allah Amrehemu Kua Uzushi Umegawanyika Sehemu Mbili : “ Mzuri Na Mbaya “ ??

-Anajibu Luqman : Anasema Ibn Kathir Allah Amrehemu : “ Uzushi Umegawanyika Sempuli Mbili : 1. Kuna Wakati Uzushi Unakua Ni Wa Kisheria , Kama Alivyosema Mtume Sala Na Amani Zimfikie : Kila Chenye Kuzuka Ni Uzushi , Na Kila Uzushi Ni Upotofu . 2. Na Kuna Wakati Uzushi Unakua Wa Kilukha , Kama Alivyosema Kiongozi Wa Waumini Omar Allah Amridhie Kuwakusanya Kwenye Sala Ya Tarawehe……. “ Tazama Tafsir Ibn Kathir Suratul Baqarat Aya Ya 117 .

Anasema Ibn Rajab Allah Amrehemu : “ Ama Yaliyopatikana Kwenye Maneno Ya Wajawema Waliyotangulia Kwenye Kupendezeha Baadhi Ya Uzushi , Hakika Huyo Ni Katika Uzushi Wa Kilukha Na Wala Si Wakisheria , Kama Qauli Ya Omar : Neema Ya Uzushi Ni Huyu…… “ Tazama Jaami’ Al Ulum Wal Hikam 28 .

_ Na Kama Tutasema Kua Kakusudia Kisheria , Kumbuka Mtume Sala Na Amani Zimfikie Amesema : “ Kila Uzushi Ni Upotofu “ Na Maneno Yake Yanayangulizwa Kabla Ya Maneno Ya Yeyote , Anasema Imam Shafii Allah Amridhie : “ Waislamu Wote Wamekubaliyana kwamba yeyote ambaye ameona Sunnah ya Mtume wa Mwenyezi Mungu iko wazi kwake, haijuzu kwake kuiacha kwa ajili ya maoni ya yeyote “ Tazama Ilam Al Muwaqiina 2/282 .

Anasema Ibn Abbas Allah Amridhie : “ Hakuna yeyote ambaye maoni yake hayakubaliwi au kuachwa isipokuwa Mtume Sala Na Amani Zimfikie “ Tazama Fatawa Assubkiy 1/138 .

_ Anasema İmam Shafii Allah Amrehemu Anasema : “ من استحسن فقد شرع “ Anasema Al-Ruwayani Maana yake : “ Anajiwekea sheria isiyokuwa sheria ya Mteule “ . Hiyi İnatuonesha Kua <u>Uzushi Mzuri Aliyo Kusudia Alimaanisha “ Uzushi Wa Kilukha “</u> .

Anasema Ibn Hajar al-Haytami – ambaye ni miongoni mwa waliogawanya Uzushi katika makundi matano – : “Uzushi Wa kidini

ni upotofu, kama alivyosema Mtume Sala Na Amani Zimfikie na miongoni mwa wanavyuoni walioigawanya katika kheri na si kheri, bali waligawanya bid'ah ya lugha tu " Tazama Alfatawa Al Hadithiyat 200 .

Anasema Ibn Hajar al-Asqalani Allah Amrehemu : "Ama 'bid'ah ni wingi wa 'bid'ah' ambayo inarejelea kitu chochote ambacho hakina mfano wa awali. Kilugha kinajumuisha kile kinachosifiwa na kinacholaaniwa, na katika desturi ya watu wa sheria ya Kiislamu, ni makhsusi kwa kile kinacholaaniwa. Iwapo itatumika katika muktadha wa kitu kinachosifiwa, basi kinatokana na maana yake ya kilugha " Tazama Fathul Bariy 13/340 .

-Anasema Omar: Ahsante , Vile Vile İmekuja Hadith Ya Mtume Sala Na Amani Zimfikie Anasema : " Kitu Ambacho Waislamu Watakiona Ni Kizuri , Na Kwa Allah Ni Kizuri …" Kaipokea Ahmad , Je Hiyi Sini Dalili Tosha Ya Kuonesha Kua Kuna Uzushi Mzuri ??

-Anajibu Luqman : Anasema Ibn Abdil Hadiy : " İmepokewa Kwa Kuinuliwa Kwa Mtume Kutoka Kwa Anas Kwa İsnad Ambayo Kuna Mtu Kaanguka , Na Sahihi Ni Mawquf – Maneno Ya - Kwa Ibn Mas'ud " Tazama Kashfu Al Khafai Cha Ajlun 2/245 .

_ Pia " الـ " Katika Athar ما رآه المسلمون Waislamu Wanaokusudiwa Hapo Ni Masahaba, Sababu Ibn Mas'ud Allah Amridhie anasema Katika Athari Hiyo : " ….Kisha Allah Akatazama Nyoyo Za Waja Baada Ya Moyo Wa Muhammad , Akakuta Nyoyo Za Masahabaze Ni Bora Za Nyoyo Za Waja ……" .

Pia Unaweza Ukasema " الـ " Katika Athar Makusudio Ni Makubaliyano , Kama Alivyosema Al Izu Bn Abdil Salam : " Kama Hadith İtakuwa Ni Sahihi , Makusudio Ya Waislamu Ni Watu Wa İjmaa- Makubaliyano – Na Allah Ndie Mjuzi " Tazama Fatawa Ya Al izu Bn Abdil Salam Karatasi 42 Namba 9 .

-**Anasema Omar:** Umesema Hadith “ Kila Uzushi Ni Upotofu “ , Na Allah Anasema : “ Unaangamiza kila kitu kwa amri ya Mola wake Mlezi , Wakawa hawaonekani ila nyumba zao tu Hivyo ndivyo tuwalipavyo wakosefu “ Suratul Ahkaf Aya Ya 25 . Je Kwanini Hapo Neno “ Kila “ Haikuangamiza Kila Kitu ??

-Anajibu Luqman : Aya Hiyo Imekhusishwa Kwa Qauli Ya Allah : “ Wakawa Hawaonekani Ila Nyumba Zao “ , Pia Umeangamiza Yale Yaliyo Amrishwa Kuangamiya .

-Anasema Omar: Abu Bakar Swidik Na Omar Allah Awaridhie Wamefanya Uzushi Wa Kukusanya Quran ??

Anasema Luqman : Anasema Rasulullah Sala Na Amani Zimfikie : “ Wafwateni Waliyokuja Baada Yangu Mimi : Abu Bakar Na Omar ..” Imepokewa Na Ahmad 23293 Na Tirmiziy 3662 . Je Hadi Hapo Unaweza Ukajifkiria Kua Abu Bakar Na Omar Allah Awaridhie Kua Wamezusha Jambo ??

-Anasema Omar: Hapana , Jambo Walilolifanya Sio Uzushi .

-**Anasema Omar:** Shukran , Nimefaidika Kua Katika Dini Hakuna Uzushi Mzuri , Bali Kila Uzushi Ni Upotofu . Ni Ngeomba Unipambanulie Hizi Dalili .

Je Ni Kweli Dalili Hizi Zina Ashiria Uhalali Wa Kusherehekea Uzao Wa Mtume Sala Na Amani Zimfikie??

-Anasema Omar: Allah Ameruhusu Watu Kufurahiya Uzao Wa Mtume Sala Na Amani Zimfikie , Allah Anasema : “ Sema: Kwa fadhila Ya Allah na rehema yake Basi nawafurahi kwa hayo , Haya ni bora kuliko hayo wanayo yakusanya “ Suratu Yunus Aya Ya 58 . Neno “ Rehema “ Makusudio Ni Uzao Wa Mtume .

-Anasema Luqman : Neno “ Rehema “ Makusudio Si Kwa Uzao Wa Mtume Sala Na Amani Zimfikie , Anasema Ibn Qayyim Allah Amrehemu : “ Yamezunguuka Maneno Ya Wajawema Waliyotangulia Kua Hakika (Sema Fadhila Ya Allah Na Rehema) Hiyi Aya Ni : Uwiislam Na Sunna “ Tazama İjtima’ Al Juyush al İslamiyyat ala Ghazwi Al Muatwila Wal Jahmiyat 8 .

Vile Vile Ukatazama Ndani Ya Quran Utakuta Allah Anasema “ Nasi hatukukutuma ila uwe ni Rehema kwa walimwengu wote “ Suratul Anbiyai Aya Ya 107 , Na Mtume Sala Na Amani Anasema : “…..Hakika Nimetumwa Kama Rehema “ Imepokewa Na Muslim 259 .

-Anasema Omar: Nimeelewa Kua Makusudio Ya Aya Hiyo Sio “ Uzao Wa Mtume “ Bali Ni “ Sunna “ . İla Kuna Aya Ambayo İmeruhusu Kukusanyika Huku Wanakumbushana Maisha Ya Mtume Hata Kama Hawatoita Uzao Wa Mtume Wakaiita “ Kongamano “ , Na Aya Hiyo Ni : “ Na tulimtuma Musa pamoja na miujiza yetu, tukamwambia: Watoe watu wako kwenye giza uwapeleke kwenye mwangaza. Na uwakumbushe siku za Allah , Hakika katika hayo zipo ishara kwa kila mwenye kusubiri akashukuru “ Suratu İbrahim Aya Ya 5 .

-Anasema Luqman : Mujahid Allah Amridhie Ametafsiri “ Siku Za Allah “ Ni : Neema Za Allah . Tazama Tafsir Attwabariy 6/861 .

Vile Vile Kama Jambo Hilo Ni Fursa Ya Kukumbushana Historiya Ya Mtume Sala Na Amani Zimfikie , Basi Qarne Tatu Bora Na Maimamu Wa Kubwa Wa Hadith Hawange Hafilika Hilo Jambo .

-Anasema Omar: Allah Akubarikini , Hapa Sasa Naona Ndani Ya Quran Hakuna Aya Yoyote Inayoruhusu Kusherehekea Uzao Wa Mtume Sala Na Amani , Ao Kugeuza Jina Kinyume Na Kusherehekea Uzao Wa Mtume Sala Na Amani Zimfikie ukaiita “ Kongamano “ .

-Anasema Omar: kuna Hadith Tele Zenye Kuruhusu Kusherehekea Uzao Wa Mtume Sala Na Amani Zimfikie , Mtume Sala Na Amani Zimfikie : “ Aliulizwa Kuhusu Funga Ya Siku Ya İjuma Tatu , Akasema : Ndio Siku Nilio Zaliwa ….. “ .

-Anasema Luqman : Subhanallah , Hiyo Hadith Hairuhusu Mtu Kusherehekea Uzao Wa Mtume Sala Na Amani Zimfikie , Niskilize Kiumakini :

Hicho Ni Kipimo Umekifanya , Na Kipimo Pindi Kikihongana Na Sunnah İliyoachwa Kipimo Hicho Ni Batwil . Mtume Sala Na Amani Aliswaumu Na Wala Hakusherehekea Uzao Wake Wakuzalia , Kumbe Kufanya Kipimo Cha Kusherehekea Uzao Wake Kipimo hicho Ni Batwil .

Hadith Hiyo İnasababu Yingi , Zimekuja Katika Riwaya Tofauti Kama “ Ndio Siku Nitakayo Fia , Ndio Siku Vitendo Vinapandishwa Mbinguni ,……” , Kwanini Mtu Uchukuwe Sababu Moja Na Zingine Uziache ??

-Anasema Omar: Nimeelewa , Na Je Hadith : “ Hakika Mtume Sala Na Amani Zimfikie Alijifanyiya Akika Baada Ya Kupewa Utume “ Inaashiria Kusherehekea Uzao Wa Mtume Sala Na Amani Zimfikie ???

-Anasema Luqman : İnastabisha Kuskia Hadith Hiyo , Sababu :

Hadith Hiyo İmepokelewa Na Bayhaqi Na Bayhaqi Pamoja Na İmam Ahmad Na Annawawiy Wameidhohofisha , Kwenye İsnad Kuna “ Abdullah Bn Muharar “ Ni Matruk .

Akika Ni Kitu Kingine , Na Kusherehekea Uzao Wa Mtume Sala Na Amani Zimfikie Ni Kitu Kingine .

-Anasema Omar: Allah Azidi Kukunawirisha Uso Wako , Na Je hujaona Kua Ndani Ya Sahihi Al Bukhari Kua : “ Abu Lahb Anapunguziwa Adhabu Siku Ya İjuma Tatu Kwa Kumuacha Uhuru Thaalabat , Sababu Thaalabat Alifurahia Uzao Wa Mtume Sala Na Amani Zimfikie “ ??

-Anasema Luqman : Hiyo Hadith Huwezi kuipata Ndani Ya Sahih Al Bukhari Kwa Matamshi Hayo , Na Ndani Ya Sahih Albukhari Hakuna Matamshi Ya “ Kupunguziwa Adhabu Kisa Alifurahia Uzao Wa Mtume Sala Na Amani Zimfikie “, Na Pia:

Hiyo Athar Uliyoileta Ni Mursal Ya Urwa, Na Mursal Hiyo Ni Dhaifu .

Sote Twatambua Kuwa Hukmu Za Kisheria Hazichukuliwi Katika Ndoto .

Kwa Faida Zaidi : Hadith Ya :

Funga Ya Ashura : Siku Ya Ashuraa İlikua İnajulikana , İla Tariki Ya Kuzaliwa Kwa Mtume Sala Na Amani Zimfikie Haijulikani Sababu Hakuna İsnad Sahihi İnayo Ashiria Jambo Hulo . Na Pia Mtume Sala Na Amani Zimfikie Aliswaumu Na Wala Hakusherehekea Uzao Wake , Kumbe Kipimo Hicho Ni Batwil .

Hadith : “ Bora Ya Masiku Yenu Ni Siku Ya İjuma , Ndipo Alipo Umbwa Adam , Na Ndipo Alipofariki ……” , Hiyi Pia İnasababu Nyingi Kama “ Ndio Siku Alitolewa Pepuni , Ndio Siku Alitubia , Ndio Siku Qiyama Kitasimama ,…..” Kwanini Mtu Uchukuwe Sababu Moja ???

-Anasema Omar: Alhamdulillah , Nimeelewa Kua Ndani Ya Quran Na Sunna Hakuna Ruhusa Ya Mtu Kusherehekea Uzao Wa Mtume Sala Na Amani Zimfikie . Na Je Unafahamu Kuwa Kuna Mambo Ya Usulul Fiqhi Yanaruhusu Kusherehekea Uzao Wa Mtume Sala Na Amani Zimfikie ???

Je Usulul Fiqhi İnaruhusu Jambo Hili ??

-Anasema Omar: Kusherehekea Uzao Wa Mtume Sala Na Amani Zimfikie Ni Katika المصلحة المرسلة .

-Anasema Luqman : Subhanallah , Tambua Mazingatio Ni Uhakika Wa Jambo Na Sio Majina , Ukitazama Uhakika Wa Kusherehekea Uzao Wa Mtume Sala Na Amani Zimfikie Utakuta İnaingia Kwenye Qauli Ya Mtume Sala Na Amani Zimfikie : “ Atakae Zuwa Jambo Ambalo Halimo Katika Dini – Sheria Yetu – Litakataliwa “ İmepokewa Na Bukhari 2697 Na Muslim 1718 .

-Anasema Omar: Na Je Kusherehekea Uzao Wa Mtume Sala Na Amani Zimfikie Ni Katika Mambo Ambayo ما لا يتم الواجب إلا به فهو واجب - Chochote kinachohitajika ili wajibu utekelezwe yenyewe ni wajibu. - ??

-Anasema Luqman : Hapo Unaashiria Kua Kusherehekea Uzao Wa Mtume Sala Na Amani Zimfikie Ni Wajibu Sababu Ni Njia Ya Kukufanya Ukampenda Mtume Sala Na Amani Zimfikie .

Swali : Je Masahaba Na Wanafunzi Wa Masahaba Na Wanafunzi Wa Wanafunzi Wa Masahaba Wameacha Jambo La Wajibu , Ambalo Ni Kushereheka Uzao Wa Mtume Sala Na Amani Zimfikie ???

-Anajibu Omar: Subhanallah , Haiwezekani Masahaba Na Wanafunzi Wa Masahaba Na Wanafunzi Wa Wanafunzi Wa Masahaba Kuacha Jambo La Wajibu Ambalo Ni Kusherehekea Uzao Wa Mtume Sala Na Amani Zimfikie .

-Anasema Luqman : Sote Twafahamu Kua Njia Zinasharti Zake :

1. Njia Hiyo İwe Ni Sheria , Na Wala İsiwi Ni Njia Ya Uzushi .
2. Njia Hiyo İsiwe İmepatikana Zama Za Mtume Sala Na Amani Zimfikie , İla Pawe Dalili Ambazo Ni عامة Za Ujumla Zenye Kuonesha Njia Hiyo .

3. İsiwe Njia Hiyo Ni Sababu Ya Watu Kupuuza Njia Ya Halali .

-**Anasema Omar:** Allah Akubarikini , Nimeelewa pia Nahitaji Majibu Ya Suala Hili La Mwisho .

Je Mbona Wanawaelimu Wanakwenda kwenye Uzao Huyo ??

-**Anasema Omar : Tunaona Wnawaelimu Wanakwenda Kwenye Uzao Wa Mtume Sala Na Amani Zimfikie , Bali Watu Wengi Wanakwenda Kusherehekea Uzao Wa Mtume Sala Na Amani Zimfikie , Je Hii Si Hoja Yenye Kuruhusu Uzao Huyo ??**

-Anasema Luqman : Tambua Allah Akulinde , Hoja Ni Allah Na Mtume Wake Kasema Nasio Kwasababu Flani Kasema , Pia Vitendo Vya Wanawaelimu Sio Hoja Hadi Vitendo Hivo Vishindikizwe Na Dalili , Na Tumeona Hakuna Dalili Yoyote İnayoruhusu Uzao Wa Mtume Sala Na Amani Zimfikie .

Ama Watu Kuwa Wengi Kwenye Uzao Huyo Hiyo Pia Sio Hoja , Allah Anasema : “ Na ukiwat'ii wengi katika hawa waliomo duniani watakupoteza na Njia ya Allah …. “ Suratul An’am Aya Ya 106 .

-Anasema Luqman : Ewe **Omar** , Mimi Na Wewe Kama Tunampenda Allah Na Mtume Wake Sala Na Amani Zimfikie , Tutambuwe Kuwa Mapenzi Yanakuwa Kwa Kumfwata Mtume Sala Na Amani Zimfikie Na Sio Kufanya Yale Ambayo Hayana Mashiko Katika Dini , Allah Anasema : “ Sema: Ikiwa nyinyi mnampenda Mwenyezi Mungu basi nifuateni mimi, Mwenyezi Mungu atakupendeni na atakufutieni madhambi yenu. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kufuta madhambi na Mwenye kurehemu “ Suratu Al İmran Aya Ya 31 .

Na Anasema Mtume Sala Na Amani Zimfikie : “ Atakae Zuwa Jambo Ambalo Halimo Katika Dini – Sheria Yetu – Litakataliwa “ İmepokewa Na Bukhari 2697 Na Muslim 1718 .

-Anasema Omar: Alhamdulillah , Nimebainikiwa Haqi Na Allah Atujalie Tuwe Miongoni Wa Wenye Kufwata Mwenendo Wa Mtume Sala Na Amani Zimfikie , Na Atuweke Mbali Na Uzushi .

Hapa Ndipo Mazungumzo Yanapoishia , Na Allah Atuweke Mbali Na Uzushi , Na Sala Na Amani Zimfikie Mtume.



MAZUNGUMZO

BAINA YA LUQMAN NA OMAR KUHUSU KUSHEREKEA UZAO WA MTUME SALA NA AMANI ZIMFIKIE

MTUNZI

ALFUQAYYIR

ABUU HUDHAYFAT BN ASHURAA

DESIGNER AND PRINTER

ABUU MANSOUR ISSA BNU ISSA